**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BUNGE LA TANZANIA**

**Simu: +255 26 2322761-5**
**Fax No. +255 26 2324218**
**E-mail: cna@bunge.go.tz**

**Ofisi ya Bunge,**
**10 Barabara ya Morogoro,**
**S. L. P. 941,**
**40490 Tambukareli,**
**DODOMA**

## TAARIFA KWA UMMA

Kamati tatu (3) za Kudumu za Bunge zinawaalika wadau kwa ajili ya kupokea na kusikiliza maoni yao (Public Hearing) kuhusu kanuni na miswada ya sheria siku ya I**jumaa tarehe 07 Agosti 2026, Jumatano tarehe 12 Agosti 2026, na Alhamisi tarehe 13 Agosti 2026, saa 4:00 asubuhi katika Ofisi ya Bunge Jijini Dodoma.** Kanuni na miswada ya Kamati hizo ni kama ifuatavyo:-

**a)** Kamati ya Sheria Ndogo itapokea maoni ya wadau kuhusu **Kanuni za Mbolea, Tangazo la Serikali Na. 68/2026, tarehe 7 Agosti, 2026** katika **Ukumbi namba 37**, uliopo Jengo Dogo la Utawala.

**b)** Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria itapokea maoni ya wadau kuhusu **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2026 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2) Bill, 2026), tarehe 12 Agosti, 2026** katika **Ukumbi wa Frank Mfundo,** uliopo ghorofa ya tano katika Jengo Kuu la Utawala.

**c)** Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo itapokea maoni ya wadau kuhusu **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kilimo wa Mwaka 2026 (The Agricultural (Amendments) Bill, 2026; na Muswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto wa Mwaka 2026, tarehe 12 na 13 Agosti, 2026** katika **Ukumbi wa Msekwa D,** uliopo Jengo la Pius Msekwa.

Kwa kuzingatia umuhimu wa kanuni na miswada hiyo, Kamati zinawaalika wadau wote kufika kwenye Mkutano huo na kuwasilisha maoni kabla hayajapelekwa katika hatua nyingine.

Aidha, maoni yanaweza kuwasilishwa kwa njia ya posta kupitia anuani ya Ofisi ya Bunge au kupitia Barua pepe ya ***cna@bunge.go.tz*** na ***kamati@bunge.go.tz .***

Kanuni na miswada hiyo inaweza kupakuliwa katika Tovuti ya Bunge ***https://www.bunge.go.tz/bills-list.***

**Imetolewa na:** Kitengo cha Mawasiliano na Elimu kwa Umma,
Ofisi ya Bunge,
S.L.P 941,
DODOMA.

**20** Julai, 2026